ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
43.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
44.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
45.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
47.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
48.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
49.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake

50.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

51.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

52.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

53.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

54.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

55.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

56.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

57.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

58.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

59.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

61. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

66.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

69.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

70.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

71.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

76.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nane – Tarehe 19 Oktoba, 2012

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 48

Ardhi na Uwekezaji Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (*ZIPA*) imekuwa ikilalamika juu ya kuwepo kwa tatizo la ukosefu wa maeneo ya ardhi kwa ajili ya wawekezaji kisiwani Pemba kutokana na serikali kuzuia maeneo ya ardhi kwa ajili ya kazi ya utafiti na uchimbaji wa mafuta.

(a) Je, suala hili lina ukweli kiasi gani na kama kweli serikali imezuia maeneo ya fukwe kwa uwekezaji wa hoteli za kitalii. Je, ni maeneo mangapi yametengwa kwa kazi za utafiti na uchimbaji wa mafuta Pemba.

(b) Kwa kuwa sekta ya utalii ina mchango mkubwa katika pato la taifa na fedha za kigeni uamuzi huo umezingatia vipi maendeleo ya Sekta ya Utalii kisiwani humo.

(c) Wawekezaji wangapi wamejitokeza kisiwani humo kuanzisha vitega uchumi vyao na kushindwa kufanikiwa kutokana na tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo) – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 48 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, mnamo mwezi Disemba 2008, Mamlaka ya Uwekezaji ilipokea nakala ya barua kutoka kwa Mhe. Waziri anaeshughulikia ardhi yenye maelekezo kuwa kuna maeneo matatu kutoka Kisiwa cha Pemba ambayo serikali imeona ni busara kutoruhusu uwekezaji wa aina yoyote kutokana na sababu mbali mbali lakini kubwa ikiwemo hiyo ya utafiti wa mafuta na gesi asili. Maeneo hayo ni Tundaua, Pujini na Ras Kiuyu Kigomasha.

   Hata hivyo, wizara haina mamlaka ya moja kwa moja juu ya masuala ya utafiti wa mafuta na gesi asilia, hivyo si kama tulilalamika kwamba hatua hiyo imechukuliwa na serikali aa, ukweli ni kwamba maeneo yaliyotengwa yalitengwa kwa kazi hiyo kwa makusudi na kwa dhamira nzuri tu ili kuepusha migongano ya hapo baadae. Na kama wizara moja imefanya basi wizara nyengine lazima iheshimu uamuzi huo. Kutokana na hayo Mamlaka ya (*ZIPA*) haikuwa ikilalamika kama alivyosema bali ilikuwa ikitoa taarifa juu ya suala hilo wakati ilipotakiwa.

b) Mhe. Spika, kwa kuzingatia mchango mkubwa wa Sekta ya Utalii kwenye pato la Taifa na fedha za kigeni, mnamo mwezi wa Oktoba 2010, *ZIPA* ilipeleka mapendekezo kwa Mhe. Waziri anaeshughulikia na ardhi na kuelekezwa kwamba wawekezaji washauriwe kuyatumia maeneo mengine ya fukwe ya Kaskazini ikiwa pamoja na Tumbe, Micheweni maeneo huru na ukanda wa Wambaa, Kiuyu Minungwini na Kiuyu Maziwang'ombe.

c) *ZIPA* huwa inawajulisha na kuwaelekeza wawekezaji ambao wanapitia hapo kuulizia maeneo ya uwekezaji katika Kisiwa cha Pemba. Kwa wale wawekezaji ambao maombi ya miradi yao haipitii *ZIPA*, basi inakuwa ni vigumu kuweza kuwajua ni wepi ambao wameenda kwenye maeneo hayo na kukosa eneo la kuwekeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri kuna taarifa hata hayo maeneo yaliyotengwa kuna baadhi yamechukuliwa. Je, ni kina nani waliochukua sehemu hiyo.

Pili, kwa kuwa suala la utafiti wa mafuta ni jambo ambalo linasubiriwa na wananchi kwa hamu ndani ya Baraza hili pamoja na wananchi nje ukiwemo wewe Mhe. Waziri. Ni lini utekelezaji huo utaanza.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo): Mhe. Spika, sina hakika hii taarifa aliyotupa Mhe. Jaku, lakini acha kwa sababu kama yeye ni Mwakilishi na Mjumbe wa Kamati atakuwa haya ameyapata *field* basi mimi kama wizara na serikali nitayachukua na tutakwenda kuyafanyia kazi. Lakini hatupendi tuwabughudhi au tuwapatishe shida wawekezaji wetu. Kwa hivyo, tunachukua kauli yako na tutakwenda kuifanyia kazi.

Kuhusu suala la mafuta nafikiri mengi tumeshayazungumza na niseme kwamba kama Mhe. Mwakilishi sitaki tena kuyaanza hapa, nafikiri maelezo mengi yameshatolewa, mikakati mingi ishatolewa na msimamo wa serikali umeshatolewa. Kwa hivyo, namuomba awe na subira hizo juhudi wakati zikiendelea kuchukuliwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri katika jibu lake amesema kwamba kuwa serikali sasa hivi haina sheria ya moja kwa moja ya kuweza kufanya utafiti wa mafuta. Je, Mhe. Waziri haoni kuwa kutokana na kuwa sheria hatuna serikali hatuoni iko haja sasa hivi maeneo hayo tukawarejeshea wenyewe wananchi ili wakawapa wawekezaji wao kwa kupata maendeleo zaidi kuliko kungojea sheria ije ya kuchimba mafuta.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo): Mhe. Spika, kama Mwakilishi naomba nimkumbushe Mhe. Makame Mshimba kwamba ardhi yote ni mali ya serikali. Hili naomba walitambue na atujulishe na afahamu vizuri. Kwa hivyo, panapohitajika mipango ya maendeleo popote pale basi serikali itachukua taratibu zake kuona kwamba mipango ya maendeleo hiyo pamoja na uchimbaji wa mafuta na uendelezaji mwengine kuona kwmaba linafanikiwa na hao waliyonao katika sehemu hiyo basi serikali itachukua utaratibu uliopo.

Lakini ninachosema kwa hatua ya mwanzo ilivyofanywa ili kuondoa migongano pale ambayo tushanusa pana mwelekeo basi acha tumuhifadhi mule, watu maeneo mengine ya uwekezaji yapo, hayo tena wawekeze huko ili tusubiri huku, hayana muda haya mafuta Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, moja kati ya fukwe nzuri na ya kisasa ni ile fukwe iliyoko eneo la Kuji Mtangani Jimbo la Kiwani. Fukwe hii iliwahi kufikwa na mwekezaji mmoja lakini akaambiwa kwamba imetengwa kwa ajili ya utafiti wa mafuta, lakini hatimaye mwekezaji mwengine akapewa na ushahidi wa hati hizo zipo. Sasa hebu Mhe. Waziri atwambie sasa na awambie wananchi wa Jimbo la Kiwani hasa eneo la Mtandani fukwe hii ni kwa ajili ya mafuta au ni kwa ajili ya mtu maalum aliyepewa hati kwa ajili ya uwekezaji ambao sasa ni miaka zaidi ya saba haijaendelezwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Mkaazi, Maji na Nishati (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo): Mhe. Spika, kama kuna eneo ambalo lilitengwa kwa ajili ya utafiti wa mafuta na likaambiwa lingojee lisijengwe na kama kuna ofisa wangu amechukua juhudi ya kulitoa eneo hilo basi eneo hilo nitalifuta litabakia kuwa ni eneo la mafuta kama kawaida. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 66

Ujenzi wa Barabara Wete-Konde

Mhe. Suleiman Hemed Khamis – Aliuliza:-

Barabara ya Wete-Konde ni barabara ambayo ujenzi wake umepindukia ule muda waliokubaliana baina ya Kampuni ya ujenzi na serikali.

(a) Mhe. Waziri ni sababu zipi hasa zilizokwamisha kuendelea kwa ujenzi wa barabara hiyo usifikie kiwango cha lami.

(b) Kama kuzorota kwa ujenzi wa barabara hiyo unatokana na udhaifu wa kampuni ya ujenzi na ukosefu wa nyenzo zilizodhoofisha utendaji. Je, wizara yako itachukua hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 66 lenye vifungu a, na b kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba muda wa mwanzo uliowekwa ili kukamilisha ujenzi wa barabara ya Wete-Gando na Wete – Konde umepindukia (mkataba ulikuwa miézi 29 kuanzia tarehe 1 Septemba, 2009 mpaka tarehe 31 Januari 2012). Muda huu umepindukia na bado barabara haijakamilika.

(a) Mhe. Spika, sababu zilizokwamisha kukamilika kwa mradi huu kwa muda uliopangwa ni pamoja na kuchelewa kulipwa fidia za nyumba na huduma kama vile uondoshaji wa laini za maji, simu, umeme na kadhalika. Aidha, kumcheleweshea malipo Mkandarasi pia nako kumesababisha ikiwa pamoja na mkandarasi kubadilisha wafanyakazi pamoja na wataalamu na upungufu wa vifaa.
(b) Kama tulivyoeleza hapo awali kudhorota kwa mradi huu ni mapungufu kwa pande zote mbili mjenzi na mjengewa, lakini imani yetu kwamba mkandarasi atajidhatiti kukamilisha mradi huu kwa muda uliosalia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu a, b na c.

(a) Mhe. Spika je, utiaji wa lami katika barabara ya Konde unategemewa kuanza lini.
(b) Kutokana na historia ya udhaifu wa shughuli za ujenzi wa barabara hapa Unguja na Pemba je, wizara inategemea kumpa *tender* nyengine mkandarasi huyu.
(c) Ni miaka mingapi imepita baada ya mkataba wa makubaliano ya ujenzi wa barabara baina ya serikali na mkandarasi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, suala la kwanza alitaka kujua ni lini barabara hiyo itawekwa lami? Mhe. Spika, hadi muda huu tunaozungumza katika barabara ya Konde tayari mjenzi ameshaweka kifusi cha kwanza na cha pili kwa kilimota 13 na *base* kwa kilomita saba. Ni imani yetu kwamba alikuwa ana mapungufu ya mtambo wa kusaga kokoto tayari mtambo umepatikana, tuna matumaini kwamba katika hizo kilomita saba ambazo ameshamalizia *base* ana uwezo wa kuweka lami muda wowote. Tutakachokifanya sisi tutahakikisha kwamba anatimiza wajibu wake huo haraka iwezekanavyo ili kunusuru eneo lile ambalo amelipata lisijelikaharibika. Sasa lini hatuwezi kutamka siku, tutachokifanya sisi tutamsisitiza anusuru muda uliosalia ili kunusuru mradi huo.

Suala la pili lilikuwa linahusiana na suala la kumpa *tender*. Mhe. Spika, utaratibu wa utoaji wa zabuni hatuwezi kusema kwamba leo hatumpi ama tutampa, kila zabuni na taratibu zake na atakayeshinda zabuni kwa mujibu wa taratibu na sheria husika ndiye atakayeshinda zabuni hiyo. Hakuna upendeleo katika zabuni hizo wala hakuna maamuzi kabla ya zabuni yenyewe kutangazwa.

Suala la tatu alitaka kujua ni muda gani ambao umezidi. Kwa mujibu wa mkataba wetu kazi hii ilitakiwa ikamilike tarehe 31 Januari, 2012. Kwa hivyo, *extention* iliyoongezeka sasa hivi kuna kipindi cha miezi kumi imeongezeka kutoka ile tarehe ambayo tulikubaliana awali mradi huu uwe umekamilika. Sababu za kuchelewa kwa mradi tumezieleza katika msingi wa majibu ya suala lake la msingi alilotuuliza.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, inasemekana kuwa msimamizi wa barabara ile ni ndani ya miezi saba au minane hajalipwa mshahara wake, na kwa maelezo yake anasema anashindia madafu. Je, habari hii ni kweli.

Pili, kwa sababu barabara ile imechelewa sana kutokana na muda uliopangwa na kuwa kila siku wanaanza upya. Je, Mhe. Naibu Waziri haoni kuwa hivyo ni kuitia serikali hasara.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tumeeleza kwamba katika matatizo yanayosumbua mradi huu ni pamoja na mjenzi kutokuelewana au kutokuendana na baadhi ya wataalamu wake, yumkini inawezekana ikawa msimamizi ana hayo matatizo ambayo ameyaeleza Mhe. Mwakilishi. Lakini sisi kama wizara matatizo hayo *oficial* hayajatufikia. Tunaomba kama kuna matatizo hayo atuandikie sisi tutachukua jitihada ya kukaa na mkandarasi huyu ili kunusuru hiyo hali kwa kuamini tu kwamba kunusuru hali hiyo kutatuwezesha mradi wetu kwenda kwa haraka ili wananchi waweze kupata yale matunda waliyoyategemea ya huduma ya barabara.

Suala la pili ni kweli kwamba kama barabara hii haikukamilika kwa muda uliokusudiwa serikali itakuwa imekula hasara. Tutahakikisha kwamba tunambana iwezekanavo mkandarasi akamilishe ujenzi wa barabara hii ili yale malengo ya serikali ya kupeleka huduma kwa wananchi wake yawe yamefikiwa.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nami nikushukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la mwisho la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri bado kuna kitu ametufunga hakijaweza kujitosheleza, muda uliosalia, muda waliokubaliana. Mimi nataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wenzake kule Tanzania Bara mawaziri tunaona wanatoa *limit date* isipofika tarehe fulani basi kampuni wanakuwa wanainyang'anya zabuni. Je, wizara yake muda gani hasa walioupanga wa kumaliza baada ya kasoro zilizojitokeza.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, suala la kujua muda gani ambao tumeupanga inatokana na mradi wenyewe ambavyo umekuwa ukienda. Mradi huu kama tulivyoeleza kwamba kuna mapungufu mengi yakiweko mapungufu ya sisi kama serikali lakini pia kuna mapungufu ya mkandarasi. Kwa mfano kama sasa hivi tukisema mradi huu ukamilike katika kipindi cha miezi sita bado sisi kama serikali tuna tatizo, ukienda upande wa Wete barabara ya Wete - Konde hadi muda huu tunadaiwa takriban shilingi 217 milioni hatujalipa fidia kwa ajili ya kumpa eneo, barabara ya Bopwe tunadaiwa shilingi 500 milioni hatujalipa fidia kwa ajili ya kumpa eneo la kufanyia kazi, eneo la Gando tunadaiwa shilingi 327 milioni hatujalipa fidia kwa ajili ya kumpa eneo, eneo la Ukunjwi tunadaiwa shilingi 37 milioni hatujalipa fidia kwa ajili ya kumpa eneo.

Sasa sisi kama serikali tutakuwa tuna fedha za kulipa fidia tukimpa eneo hilo tutakuwa tunajua kwamba kwa muda gani mkandarasi ataweza kumaliza kazi hiyo. Tunachokifanya sasa hivi ni kuhakikisha yale maeneo ambayo yameanza kufanya kazi ambayo ame…. ameweka kifusi ameshafikia kiwango cha *base* basi tunachomtaka ni kwamba akamilishe uwekaji wa lami ili tujue kwamba kuna maeneo tumeshakamilisha utaratibu mzima wa ukamilishaji wa mradi, lakini kwamba lini tutakamilisha mradi huu inategemea na hiyo changamoto ambayo iko kwa upande wetu serikali tutaweza lini kukamilisha zoezi la kumpa eneo kwa ajili ya ujenzi.

Nam. 8

Wananchi Kutokulipwa Fidia Zao

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa Kambi ya KVZ iliyopo Ndugu Kitu katika barabara ya Vikunguni katika Jimbo la Wawi imejengwa ndani ya Mashamba ya wananchi ambayo ndani yake mna miti ya kudumu kama vile Miembe, Minazi na hata kuvunjwa "*foundation*" za nyumba za makazi ya kudumu. Na kwa kuwa KVZ walivamia mashamba hayo bila hata kuwalipa fidia wananchi hao.

(a) Je, kufanya hivyo si kwenda kinyume na misingi ya Utawala Bora pamoja na Haki za Binadaamu.

(b) Mhe. Waziri atakubaliana nami kuwa, wanyonge katika nchi hii hawana haki na wenye haki ni watawala pamoja na matajiri tu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 8 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, eneo ambalo limejengwa Kambi ya KVZ iliyopo Ndugu Kitu katika barabara ya Vikunguni katika Jimbo la Wawi ni eneo la serikali ambalo lilikuwa limekatwa eka. Na wananchi ambao walipewa eka hizo wamepewa viwanja kama fidia. Mhe. Spika, wizara yangu haijapokea malalamiko yoyote ya wananchi katika eneo ambalo lilitolewa tangu kipindi hicho hadi leo.

(c) Mhe. Spika, sikubaliani na Mhe. Mjumbe kuwa wanyonge katika nchi hii hawana haki na wenye haki ni watawala pamoja na matajiri tu. Mhe. Spika, hii nchi haina watawala, hii nchi wananchi tunajitawala na ndio maana tuko hapa katika Baraza hili kwa mujibu wa Katiba tunapanga namna vya kuendesha nchi yetu kwa idhini ya wananchi waliotukabidhi kwa mujibu wa Katiba. Kwa ujumla wanyonge katika nchi hii wana haki kama raia wengine kutokana na misingi ya Utawala Bora pamoja na Haki za Binaadamu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa amekiri kwamba ardhi iliyojengwa Vikosi vya KVZ pale Ndugu Kitu ni ardhi ya serikali, na kwa kuwa vikosi vya KVZ ni vya serikali pamoja na wananchi waliokuwa wakitumia ardhi ni wa serikali, na kwa kuwa wananchi wa Mji wa Chini Dutani, Wara, Vikunguni pamoja na maeneo mengine walikuwa wakitegemea sana ardhi ile kwa ajili ya kilimo pamoja na makaazi, na kwa kuwa hakuna ushahidi unaothibitisha maneno ya waziri kwamba walifidiwa viwanja vyengine, na kwa kuwa kamati yake inayoshughulika na miundombinu Mhe. Spika, ilifika eneo lile na ikapata malalamiko ya wananchi kuhusiana na kunyang'anywa ardhi yao na serikali na baadae kupewa KVZ. Je, ni lini serikali itawalipa fidia pamoja na kwamba ardhi ni ya serikali lakini dhima zao yaliyoko katika ardhi ni yao. Je ni lini serikali itawalipa fidia wananchi wale ili waweze kukidhia yale mazao yao yakiwemo miembe na miti mingine ya kudumu.

Pili, kwa kuacha kuwalipa fidia wananchi wale je, serikali si itakuwa imedhulumu wananchi wake wenyewe.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nitaanza na hili la Pili. Mhe. Spika, serikali haina nia ya kuwadhulumu wananchi wenzake au wananchi wake mana ndio wananchi wenyewe wanaoendesha serikali hii.

Swali lake la kwanza kama liko lalamiko la fidia ambalo linaweza kuthibitishwa na kama kweli kumbukumbu zilioko hazioneshi kwamba imeshalipwa, serikali bila shaka italipa fidia hiyo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kuweza kunipa nafasi kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, ni kweli tulikwenda kama kamati pale na wananchi wakatulalamikia kuwa mpaka leo hii hatujapewa fidia ya viwanja na wala matunda. Lakini pamoja na majibu yake Mhe. Waziri hebu naomba atuhakikishie kuwa viwanja walivyopewa pale wananchi hao ni wangapi n aje, Mheshimiwa ipo haja ya kuwa sisi kama kamati kuhakikisha kuona zile hati zao zimetolewa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kama nilivyokwishakusema serikali haina nia ya kumdhulumu mwananchi haki yake na kwa sababu hiyo nimesema kama tutathibitisha kwamba kuna mwananchi anadai na ikathibitika hivyo hiyo fidia italipwa. Pia anataka nimpe kwa hesabu, hapa Mhe. Spika, siwezi kumpa orodha yote lakini itabidi niwasiliane na watu wangu ili tujue viwanja vilivyokwishakutolewa ni mahali gani nimletee kwa maandishi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba nijibu swali la nyongeza kwa nyongeza zaidi la Mhe. Makame Mshimba.

Mhe. Spika, mimi ni mwenyeji wa eneo hilo linalozungumzwa lenye urithi wetu maana marehemu baba yangu alikuwa anamiliki sehemu hiyo, na wakati hatua zikichukuliwa tulishirikishwa vizuri sana Mhe. Spika, naamini wale

wahusika wengi walipata haki zao. Lakini kama yupo kweli mtu ambaye bado hajapata haki hiyo basi ni vizuri akaleta taarifa vizuri serikali na hatua zikachukuliwa.

Lakini kwa sehemu kubwa Mhe. Spika, lilikuwa ni eneo la shamba yetu na hatukuwa na matatizo na ulipofanyika utaratibu huo tuliungana na serikali. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba uniruhusu nimuulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tayari kambi hiyo katika ujenzi wake ilikuwa ni karibu ni maeneo ya wananchi na kwa kuwa serikali ni wananchi na kwa kuwa ardhi ni mali ya serikali, jee Mhe. Waziri huoni kuna ni vizuri kuihamisha kambi ile na kuisogeza sehemu ambayo wananchi hawapo karibu nayo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ilipojengwa ile kambi haikuwa karibu na wananchi lakini wananchi wetu wana tabia ya kusogea karibu na kambi. Hali hiyo inaonekana Dunga ilikuwa ni uwanda mtupu lakini hivi sasa wananchi wamekwenda pale wanajenga nyumba za kuishi, Vitongoji ilikuwa baada ya skuli patupu pote, hivi sasa wananchi wanakwenda wanajenga nyumba za kuishi na ninategemea hapo pengine tuhihama tukenda tukishakuweka kambi tu basi na wananchi watakwenda karibu na hapo wakajenge vile vile.

Hili ni tatizo ambalo inabidi wananchi wetu kwa kweli si vizuri kukaa karibu na kambi. Karibu na kambi tumeona Gongolamboto yaliyotokezea, lakini wananchi wetu ndivyo wanavyopenda kuishi hivyo.

Hivyo ninadhani hata tukiihamisha pale tukiipeleka mahali ambapo hapana nyumba nina hakika wananchi watakwenda kukata viwanja wakae karibu na kambi

Nam. 9

Wawekezaji Kwenda Kinyume na Taratibu

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Baadhi ya Wawekezaji huomba Ardhi serikalini kwa ajili ya kuwekeza katika sekta husika, lakini baada ya kupatiwa hati miliki ya ardhi hiyo, huitumia kinyume na maombi walivyoomba kabla. Kwa mfano, badala ya kujenga shule au hospitali hujenga aidha baa, au taasisi nyengine za kidini.

Je, wizara huchukuwa hatua gani kwa wawekezaji wa aina hii.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 9 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Nambari 12 ya 1992 ndiyo inayompa mamlaka Waziri wa Ardhi ya kuweza kuwakodisha wawekezaji wa nje *"Foreign Investor"* na ndani. *"Local Investors"* kwa kuzingatia maelekezo ya vibali vyao kutoka ZIPA au Kamisheni ya Utalii. Hivyo ikitokea Mwekezaji kwenda kinyume na masharti ya mkataba wa ukodishwaji ardhi (*Land Lease Agreement*) au kuanzisha mradi kinyume na maelekezo ya ZIPA, huko ni kuvunja mkataba (*breach of contract*). Kwa mamlaka yale yale aliyopewa Waziri wa Ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Nambari 12 ya 1992, Waziri anayo mamlaka ya kuweza kufuta taratibu zilizopo kama Sheria ya Ardhi inavyoelekeza pindipo masharti ya mkataba huo yatavunjwa au mwekezaji kuitumia ardhi kinyume na maombi aliyoomba kabla.

Mhe. Spika, kuanzia mwaka 1986 – 2012, Wizara ya Ardhi imeshafuta jumla ya mikataba ya ukodishwaji ardhi (*Land Lease Agreement*) ipatayo 60 kwa sababu mbali mbali na kuvunja masharti ya makubaliano yaliyofungwa katika mikataba hiyo baina ya Serikali na Wawekezaji.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwa kuwa kuna baadhi ya wawekezaji wanaomba ardhi kuekeza kama ujenzi wa skuli na mambo ya maendeleo lakini badala yake hujenga mambo ya ibada kama vile madhabahu, misikiti pamoja na makanisa.

Jee, serikali inayo habari hiyo. Hilo la kwanza.

Pili jee serikali ina habari kwamba kuna mwekezaji aliomba kujenga *nursery school* katika ardhi ya Mfikiwa lakini kajenga Kanisa, serikali inayo habari hiyo na kama inayo habari hiyo serikali itachukua hatua gani kwa mwekezaji yule.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba amechukua *lease agreement* kwa uhakika kwamba anataka kufanya kitu fulani lakini akafanya jengine, hiyo ni *breach of contract* na inatakiwa mkataba ule uvunjwe na ardhi ile anyang'anywe.

Na kama hilo lipo alilolisema la pili kwamba kuna mtu aliomba kujenga *nursery school* lakini kajenga Kanisa, hilo suala itabidi nilifuatilie na kama lipo hicho kiwanja tutakifuta na hiyo *lease* tutaifuta.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba azidi kutuelimisha kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kutokana na baadhi ya wawekezaji kubadilisha nia ya maombi waliyopeleka kwenye wizara ama kwa kujenga Msikiti, Kanisa ama hata ma-*bars*. Mhe. Waziri anajua kwamba katika eneo la Chake-Chake kwenye Msikiti mkubwa wa Africana ambao serikali iliwaridhia wawekezaji wale au matajiri Msikiti kwa ajili ya ibada.

Sasa Msikiti huo imekuwa ni sehemu ya mgogoro baina wamiliki wa Msikiti na wananchi kutokana na kwamba wamiliki wa Msikiti wameamua kujenga uzio wa ukuta uzio ambao utasababisha mafufuriko kwa nyumba za wanyonge waliopo karibu ya Msikiti huo.

Na jee, kwa kuwa ramani ya mwanzo ambayo iliombewa ndani ya serikali sio iliyofuatwa, nini hatua ya serikali itakayokaa na matajiri na wananchi ili kuondosha mgogoro ambao unaashia vurugu wakati wowote kutokana na maamuzi hayo ya wenye Msikiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, kiwanja chochote anachopewa mtu kina *beacons* yaani mipaka ya eneo ambalo anatakiwa alitumie kwa ajili ya ujenzi ule aliokusudia na anapojenga kiutaratibu hutakiwa awasilishe ramani katika afisi maalum aeleze anataka kujenga namna gani na wataalamu wa ardhi kama pana matatizo ya maji pana matatizo ya mambo gani huwa wanatoa maelekezo nini kifanyike ili kuepuka madhara yatakayotokea baadae. Huo ndio utaratibu.

Sasa mimi ninawaomba wale wanaochukua viwanja wakajenge wasipuuze hii hatua ya pili ya kuonana na watu wanaohusika na kuitizama ile ramani ya kile kitu anachokijenga ili kutoa maelekezo ili hayo madhara yasije yakatokea. Kwa hivyo hawa wananchi wanaopata matatizo hayo ni vizuri maafisa wangu wanaohusika na masuala ya upangaji miji waende wakaitizame hiyo ardhi na watoe maelekezo halafu ukata unaweza ukajengwa lakini *access* ya kutoka maji itakuwepo na maji yatakuwa yanatoka na hapatakuwa na mafuriko kama maelezo watafuata maelekezo watakayopewa na watu wa mipango miji.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamo wa Pili: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri wa Ardhi naomba kuongezea jibu la nyongeza kama lilivyoulizwa na Mhe. Hija kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, suala hili malalamiko yake yaliletwa katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na Makamo wa Pili wa Raia aliniagiza mimi kukutana na wahusika wa pande pili, na tulifanya mkutano na wananchi wa eneo hilo na

wanaosimamia Msikiti pamoja na wataalamu mbali mbali wanaohusikana na mambo ya ardhi, mambo ya maji na wengine.

Jambo hili tumelizungumza kwa kina na tuliwaomba wananchi wetu wavute subra na serikali itatoa muongozo unaofaa kuhusu jambo hilo. Shauri lao la kwamba eneo lile linakaa maji lilisikilizwa sana na pale ilitakiwa kabisa na muongozo uliooneshwa kwamba kuna ramani na kama ujenzi wowote utafanyika, utafanyika kutokana na taratibu za majenzi.

Lakini hivi sasa serikali ilisimamisha kuendelea na ujenzi ule mpaka hapo taratibu zitakapokamilika zote za kuonekana kama ujenzi unaweza kuendelea au hauwezi kuendelea. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 62

Kilimo cha Mpunga Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu langu Nam. 62 naomba uniruhusu kusema machache.

Nimpongeze Mhe. Mtumwa Kheir ambaye muda mfupi anategemewa muda mfupi atanijibu swali langu hili kwa kuteuliwa kwake kupata nafasi ya Naibu Waziri, tulikuwa tupo wengi humu tunalilia nafasi hiyo tukisubiri kwa hamu lakini Mwenyezi Mungu hakutuandikia. Hii ni kazi ya Mwenyezi Mungu ambayo haina makosa, hii inatokana na Mtumwa Kheir kuchapa kazi wake unaonekana katika Baraza hili, mashirikiano yake haya hata Mhe. Rais kumuona na kumteua.

Mhe. Mtumwa Kheir nikupongeze sana na nikutakie kila la kheri afya njema na kazi njema. Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba swali langu Nam. 62 lipate jawabu.

Wananchi wa Zanzibar hasa katika Jimbo la Muyuni mwaka huu wameunga mkono kwa vitendo mpango wa serikali wa kuleta mapinduzi ya kilimo.

a) Serikali imejitayarisha vipi kuondoa kasoro zilizojitokeza katika msimu ujao.
b) Serikali imejitayarisha vipi na upatikanaji wa matrekta kwa muda muafaka ili kuvuka lengo la kulima hekari 40,000 msimu ujao.
c) Serikali imeweka mikakati gani ya kuhakikisha mbegu na mbolea zinawafikia wakulima mapema kabla ya kumalizika kwa msimu wa kilimo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa niaba yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 62 kama ifuatavyo.
Mhe. Spika, kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a), (b) na (c), kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo ikiwa ni pamoja na kutaja kwa ufupi baadhi ya kasoro zilizojitokeza msimu wa kilimo wa uliopita.

a) Matrekta yalichelewa kulima kwa kipindi cha siku 60 kutokana na hali ya hewa ya mvua nyingi mara tu baada ya kuanza msimu. Matrekta yalikuwa kidogo na baadhi yaliharibika mara kwa mara. Uhaba wa pembejeo ikiwemo mbolea na dawa.

b) Wakulima walichelewa kutoa michango ya mafuta na baadhi ya viongozi wa mabonde kutolewa uaminifu. Hata hivyo kwa upande wa Muyuni matatizo hayo hayakuwa makubwa kwani wakulima wa Muyuni ni miongoni waliofanikiwa vizuri kutokana na ushirikiano mzuri baina yao Wizara ya Kilimo na viongozi wa jimbo.

Aidha Wizara ya Kilimo inachukua fursa hii kuwapongeza wakulima wa Muyuni na Mtende kwa mafanikio ya kupata mafanikio mazuri kwa msimu uliopita.

Mhe. Spika, kutokana na kasoro na msimu uliopita wizara imejitayarisha kwa kuanza matayarisho mapema ambapo kwa msimu huu ukulima wa matrekta umeanza tarehe 3/9/2012 katika mabonde ya Unguja na Pemba.

Wakulima wa Muyuni pamoja na wa maeneo yote tayari wameshahamasishwa kupitia kamati zao mabondeni kujitokeza mapema kutoa michango yao ya mafuta ili walimiwe mapema.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo imepanga kuongeza idadi ya matrekta pamoja na kuandaa mipango ya dharura ya kutengeneza matrekta kwa haraka pindi yakitokea maharibiko.

Aidha serikali pia imeongeza idadi ya pembejeo ikiwemo mbolea kutoka tani 500 msimu uliopita hadi tani 1500 msimu huu mwaka 2012-2013.

Dawa ya magugu kutoka lita 20,000 hadi 30,000 na mpango wa kutoa ruzuku kwa pembejeo utaendelea.

Mhe. Spika, wizara tayari imeshaagiza pembejeo hizo kupitia zabuni za wazi na wazabuni wanatarajiwa kuleta pembejeo hizo ndani ya mwezi huu wa Oktoba. Wizara yangu inawaomba viongozi wa majimbo hasa wa Muyuni na Mtende kushirikiana kutoa michango yao mapema.

Mhe. Spika, lengo la kulima eka 40,000 limeekwa kwa madhumuni ya kuongeza uzalishaji wa mpunga kwa kupunguza uagizaji wa mchele kila mwaka. Lengo hilo ni pamoja na maeneo ya juu yatakayolimwa mpunga wa aina ya NERICA, hali hii inatokana na wananchi wengi kujitokeza kutaka kulima mpunga hasa wa NERICA na ukizingatia kwamba upatikanaji wa pembejeo asilimia kubwa ni kwa njia ya ruzuku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kwa dhati kabisa na unyenyekevu wa hali ya juu nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa ufundi wa muda mfupi tu aliouonesha katika kujibu swali langu, tukapata Manaibu Mawaziri kama hawa watatu Mhe. Spika, tutafika mbali, ikiwa huyu mara ya mwanzo katika kujibu swali hili, nimuulize swali dogo tu la nyongeza sana.

Sababu gani zilizopelekea wananchi wa Jimbo la Muyuni kulimiwa shamba lao nusu na nusu likaachwa wakati wameshakamilisha taratibu zote kabisa na vile vile wakiwa wameitikia wito wa kilimo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Mwakilishi kwa mashirikiano makubwa kwa wakulima wake wa Jimbo la Muyuni na ndipo niliposema katika jibu langu kuwa mafanikio mazuri yalipatikana katika Jimbo la Muyuni.

Mhe. Spika, watu wa Muyuni kutokana na mafanikio yaliyopatikana kwamba wamelimiwa wote na kama kuna wananchi ambao hawakulimiwa kutokana na jumuiya zao, basi mimi nipo pamoja kukaa na Mwakilishi ili kutatua suala hili.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Kwanza kabisa nampongeza Mhe. Naibu Waziri kwa kuteuliwa nafasi hii. Katika jibu lake alisema kwamba lengo ni kuongeza uzalishaji wa mpunga ili kupunguza uingizwaji wa mchele nchini. Jee, ule mpango wa kuanzisha ghala ya akiba umefikia wapi.

Mhe. Spika: Hili swali lipo nje kidogo ya swali mama kwa sababu hii ghala ya akiba si kwa zao la mpunga peke ni pamoja na mazao mengine. Nimuombe Mhe. Asha alitafutie utaratibu wa kuuliza swali la msingi.

Mhe. Farida Amour Mohamed: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali dogo la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri katika jibu lake mama alisema kwamba matrekta katika msimuu uliopita yalikuwa mabovu. Naomba kumuuliza swali. Jee, katika msimu huu matrekta mazima ni mangapi na mabovu ni mangapi kwa Unguja na Pemba ili kuondosha kasoro zilizopita katika msimu uliopita.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli nilisema kwamba msimu uliopita kulikuwa na matrekta ni dhaifu. Matrekta yaliyokuwepo Unguja mpaka hivi sasa yaliyokuwa ni mazima ni matrekta 15 na matrekta 9 ambayo yanafanyiwa matengenezo.

Kwa Pemba kuna matrekta 9 ambayo ni mazima na matrekta 4 yanafanyiwa matengenezo na matrekta 20 yataingia wakati wowote nchini.

Mhe. Nassor Salum Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, msimu uliopita kuliingizwa mbolea ambayo iliyokuwa mbovu na isiyokuwa bora. Jee, serikali ilichukua hatua gani kwa wale walioleta mbolea ile.
Pili wale walioathirika kwa kununua mbolea ile walilipwa fidia gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, suala la kuingizwa mbolea mbovu katika msimu uliopita naomba suala hili naomba aniachie nitakwenda kulifanyia utafiti halafu tutakuja kumletea jawabu lake.

Pia hatua za kuchukuliwa nalo pia tutakuja kumletea jawabu lake kwa maandishi.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri tunakushukuru sana. Ni ufundi wa aina yake.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na Kuanzishwa Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira ya Mwaka 2012

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimwa Wajumbe jana tulifikia pahala kwamba leo hii tumalize majumuisho na kwa maana hiyo basi twende moja kwa moja kwa kufanya majumuisho.
Ilikuwa tuanze na Mhe. Naibu Waziri lakini simuoni basi moja kwa moja twende kwa Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba sasa nichukue muda mchache kufanya baadhi ya ufafanuzi na kwa pale panapohitaji utaalamu wa kisheria, Mhe. Mwanasheria Mkuu yupo hapa atanisaidia.

Mhe. Spika, juzi au jana asubuhi tulipokuwa tunawasilisha sheria hii tuliona ni ndogo labda na kazi ingemaliza mara moja, lakini baada ya muda Wajumbe wakaanza kuchangia na walifika 15.

Kwa heshima yako naomba niwataje:

1. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
2. Mhe. Hassan Hamad Omar
3. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
4. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
5. Mhe. Rufai Said Rufai
6. Mhe. Ashura Sharif Haji
7. Mhe. Asha Abdu Haji
8. Mhe. Salum Abdalla Hamad
9. Mhe. Salma Mohamed Ali
10. Mhe. Mohamed Mbwana Haji
11. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
12. Mhe. Hija Hassan Hija
13. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
14. Mhe. Mohammed Haji Khalid
15. Mhe. Farida Amour Mohammed

Mhe. Spika, mingi ya mijadala ilikuwa ni maongezo ya waraka lakini hoja ya msingi ilikuwa ni hoja inayohusu wataalamu.

Kwa hivyo Waheshimiwa wengine walikuwa kama wamepata nafasi kuchangia ule mswada uliopita na kutoa ufafanuzi zaidi. Ninawashukuru kwa sababu ilikuwa inaongeza kutupa sisi wizara nafasi kuona jinsi mawazo ya waraka ule wa *Public Health* ulivyo umuhimu. Lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa yanahitaji kutolewa maelezo.

Mhe. Bikame yeye alipongeza na kuunga mkono tu. Mhe. Hassan Hamad alitoa maelezo mengi isipokuwa alikuwa anaeleza umuhimu wa kutolewa elimu ya afya, masuala ya watendaji kusomeshwa, wafanyakazi wa jamii kukaa pamoja na wananchi na kwamba Afisi zipelekwe vijijini. Suala hili la kwamba afisi zisiwepo mjini lilirudiwa sana na watu wengi. Ni vizuri nilieleza kwa ujumla kwamba hawa wafanyakazi wenyewe watakuwa wanafanya kazi huko, ni kule kwenye kazi. Mara nyingi itakuwa ni Mabaraza ya Mji na Halmashauri. Kwa hivyo hili litafanyika.

Kulikuwa kifungu nambari 33 ambacho Mhe. Abdalla Mohamed Ali alitaka kuona kwamba kifungu hiki kinahusu adhabu na adhabu zilikuwa ni tofauti. Matatizo yalikuwa ni tofauti lakini adhabu ikiwa sawa sawa.

Mhe. Spika, naomba nikisome ili Wajumbe wapate marejeo. “Endapo mtu aliyepokea wito wa Baraza wa kwenda kutoa ushahidi na kuwasilisha nyaraka kwenye uchunguzi unaofanywa chini ya masharti ya sheria hii atashindwa, hiyo ni (a) atashindwa bila ya sababu ya msingi, atakataa bila ya sababu ya msingi, atamkejeli Mjumbe wa Baraza, atakataa kutoa ushahidi”. Sasa haya ni makosa tofauti lakini *conclusion* yake ya kile kifungu ilikuwa anasema atakuwa ametenda kosa atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini.

Sasa hii faini inaonekana ilikuwa ni sawa sawa kwa makosa yote. Tumekubaliana na ushauri uliotolewa kwamba kifungu hiki tushirikiane na Mwanasheria ili kila kosa liwe na adhabu tofauti. Naomba hilo tukubaliane na Wajumbe.

Kulikuwa kifungu chengine nambari 20 ambacho kilikuwa kinazungumza habari ya mgeni kwamba mgeni huyo ni mgeni gani na kila mtu Zanzibar atakuja kupewa kitambulisho.

Mhe. Spika, naomba tutofautishe baina ya vitambulisho vya wakaazi wa Zanzibar na ugeni huu. Kila mgeni anayetaka kutoa huduma kama Afisa afya ya jamii na mazingira, atalazimika kuwasilisha nyaraka zifuatazo;

Kwa hivyo, huyu ni mgeni kulingana na sheria hii, sio mgeni kulingana na vitambulisho, na kwamba tumekubaliana kuwa huyu aelezwe na ataelezwa na bahati nzuri kwenye masahihisho haya yaliyofanywa na Kamati, basi Wajumbe wa Kamati waliongeza na kutafsiri neno ‘mgeni’ limo katika yale masahihisho. Naomba kusoma; inaingizwa tafsiri ya neno ‘mgeni’ na itasomeka;

‘Mgeni’ Maana yake ni Afisa wa Afya ya Jamii na Mazingira anayetoka nje ya Tanzania. Kwa hivyo, limetafsiriwa vya kutosha neno ‘mgeni’, kwa hivyo naomba likubalike hivyo Mhe. Spika. Kuna kifungu nambari 18 kilitakiwa kitajwe na malipo hapo kwa hapo. Kifungu nambari 18 nikikisoma Mhe. Spika, kinasema:

“Kila ombi la usajili na leseni litaambatanishwa na malipo kama linavyoamuliwa na Baraza”.

Mhe. Spika, malipo haya itabidi yabadilike na yatakuwa kwa mujibu wa sheria hii na kwa sababu thamani ya pesa inabadilika, haiwezi ikawa hayo hayo kwa muda wote. Malipo hayo yatatajwa pale kwa sababu wakati ule thamani ya pesa itakuwa inajulikana kwa wakati ule. Kwa hivyo, haiwezi ikawa iachwe kama ilivyo au ibakie hiyo hiyo kwa muda wote.

Kule kuna kifungu nambari 21 Mhe. Spika, ambacho nadhani kilikuwa kinahusu usajili wa muda. Mhe. Spika, usajili wa muda unalazimika kwa sababu inategemea mahitaji na kukimbiza usumbufu katika sheria zote zinazohusu usajili, kifungu hiki hutokeza ili kuwahudumia wale ambao wanaweza kuja wakataka kufanya kazi hii, aidha kwa utafiti au kwa muda mchache. Mara nyingi huwa tunapata mabingwa wa namna hiyo. Hata madaktari Mhe. Spika, huwa wanakuja wanafanya kazi, wakifika kufanya kazi hapa wanafika mahali wanasema kwamba kutokana na kazi hii niliyofanya, naomba basi nipewe leseni nifanye utafiti wa suala hili. Sasa baada ya kufuata ule utaratibu mrefu wa urasimu, akishakuwa yale masharti ya msingi anayo, huwa anapewa ruhusa ya muda kufanya ile kazi aliyokusudia kwa muda ule.

Mhe. Spika, kulikuwa na vifungu ambavyo vimetajwa na Wajumbe wengi, kama kifungu cha 4(c) na (d), Wajumbe wengi wamekuwa wakirudia, lakini mara nyingi ilikuwa ni masahihisho ya lugha. Hayo tunakubaliana nayo kwamba yatafanyiwa marekebisho na baada ya kutizama kwenye masahihisho haya nimegundua kwamba Wajumbe wa Kamati walikwishachukulia hatua masuala hayo.

Mhe. Spika, nikiendelea kutoa ufafanuzi mdogo wa mambo mengine, kulikuwa na kifungu nambari 11, ambacho nacho nakumbuka Mhe. Abdalla alikuwa anasema ile ni wingi wa wachache au wingi wa kura, nalo vile vile ni suala la kusahihisha. Tunakubaliana nalo kwamba ni wingi wa kura sio uchache wa kura.

Mhe. Spika, Mhe. Rufai Said Rufai yeye alitoa maelezo marefu ya jinsi matatizo haya yalivyo. Nayo tunayakubali, kwa uchambuzi wake hakuwa na suala la msingi la kutuhoji isipokuwa alikuwa anaeleza hali halisi ya matatizo ya uchafu na mazingira.

Mhe. Ashura Sharif Ali, naye vile vile alituunga mkono na akajaribu kutoa ufafanuzi kwa sababu yeye ni Mjumbe wa Kamati.

Pia Mhe. Asha alikuwa na hoja mbili zilizokuwa zinamsumbua kwamba vipi wale Wajumbe wanaotoka kwenye sehemu ya sekta binafsi watapatikana. Hawa kwa kawaida huwa tunapeleka maombi yetu kwa taasisi inayoitwa *Chamber of Commerce*. *Chamber of Commerce* ndio taasisi inayowaunganisha sekta binafsi, na wao kulingana na haja ya suala lenyewe huwa wanafanya vikao vyao na sisi kutuletea majina ya yule waliyemkubali.

Mhe. Spika, nina mfano mzuri wa hivi karibuni tulipopitisha sheria ya Mkemia Mkuu, alitakiwa mjumbe mmoja atoke kwenye *Chamber of Commerce*. Tuliwaandikia na wakatuletea mjumbe baada ya wao wenyewe kukutana. Ametoka taasisi gani huwa sisi hatujui. Isipokuwa tunachojua ni kwamba ametoka *Chamber of Commerc*e. Hivyo ndivyo utaratibu unavyofanywa, kwa hivyo kutakuwa hakuna matatizo.

Mwisho jengine alisema Mhe. Asha kwamba anaogopa masuala ya usajili na kutoa leseni yasiwe na urasimu. Hili halitokuwa na urasimu kwa sababu muhimu, masharti ya kupata leseni yalishatajwa kwenye sheria, kwamba ukitaka kupata leseni utimize masharti haya, ukishayatimiza tu yale masharti basi bodi inakaa na inabidi wakupe leseni hiyo ya kufanya kazi zako. Kwa hivyo, hakutakuwa na usumbufu.

La tatu na yeye alilirudia vile vile kutaka kuona kwamba watu hawa wanafanya kazi vijijini. Tunaomba kumthibitishia kwamba watafanya kazi vijijini.

Kuna Mhe. Salim Abdalla yeye alikwenda mbali kidogo, akazungumza hali ya mazingira yanayoambatana na taka au maji machafu kuingia baharini na kuchafua mazingira. Alikwenda mbali akasema maji yale yakifika samaki wanakula na halafu sisi tunawala samaki.

UTARATIBU

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu. Mhe. Spika, natumia utaratibu kifungu cha 72 cha kanuni yetu. Mhe. Spika, sasa hivi Mhe. Waziri wa Afya yuko mbele kuhitimisha mjadala unaohusiana na mswada wa sheria. Kanuni yetu inatuelekeza kwamba masuala haya ya kuendesha shughuli zetu hizi na kufanya maamuzi, yanahitaji Baraza letu hili angalau tutimie nusu ya Wajumbe ili tufanye maamuzi. Lakini Mhe. Spika, nasikitika sana kwa kweli kwamba hili Baraza lako lenye Wajumbe 81, basi sasa hivi Wajumbe sote tuko wajumbe 24 ni chini ya nusu ya Wajumbe.

Sasa kitendo kinachofuata ni kitendo ambacho kitahitaji Baraza lako liwe na Wajumbe zaidi ya nusu, kitu ambacho kwa kweli hatutimii. Hali hii ambayo ilidumu tangu jana. Tunakumbuka kwamba jana shughuli zetu zilisita kwa sababu hiyo hiyo na leo hali inaonekana ni hiyo hiyo na hasa wenzetu hawa wa upande wa pili wa Chama cha Mapinduzi *backbenchers*, hiki kitendo chao kwa kweli sasa hivi kinaanza kunipa mashaka.

Sasa Mhe. Spika, naomba muongozo wako katika hili.

Mhe. Spika: Kuhusu kifungu hicho ni kweli na hata Katiba inasema hivyo hivyo, kwamba hatuwezi tukafanya maamuzi kama kiwango cha Wajumbe waliomo humu ndani haijafikia nusu ya Wajumbe wote wa Baraza. Katiba

inasema hivyo, nadhani ibara ya 82 kitu kama hicho, ibara ndogo ya (2) na kanuni chini ya ibara hii ya 72 iliyosomwa.

Ni kweli kwamba na ni dhahiri kama hivyo tunavyozungumza ndivyo taratibu zilivyo. Nimemuandikia Waziri wa Nchi hivi punde kwamba hali inavyoonekana iko tete kidogo, nitaendelea kuhimiza kwamba Wajumbe waingie ndani, ikifika pahala Mheshimiwa akitoa hoja, ili kuwauliza Waheshimiwa Wajumbe na idadi ya Wajumbe hawajatimia, mimi sitowahoji nitaakhirisha kikao hiki. Kwa hivyo, wakati tunaendelea tutakuwa tunaendelea kuwahimiza Waheshimiwa Wajumbe waingie ndani ili Mheshimiwa aendelee. Wanaweza wakarudi ikafikia idadi inayohusika, nikihesabu hapa pamoja na msaada wa makatibu wangu hapa kwamba idadi ya Wajumbe haijatimia, sitohoji kwa sababu hatuwezi tukafanya uamuzi chini ya kiwango cha Wajumbe kama inavyosemwa na Katiba pamoja na kanuni zetu. Tutaakhirisha kikao tutaona nini cha kufanya hapo baadae.

Tuendelee Mhe. Waziri wa Afya. Wakati huo huo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe walioko nje waingie ndani ili tumalize kazi hii. Wahudumu wetu tuwaombe Waheshimiwa Wajumbe waingie ndani.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, Mhe. Salim Abdalla Hamad, alizungumza masuala ya maji kwenda baharini na kuchafua mazingira ya bahari na samaki wanakula na sisi baadae tunawanunua wale samaki. Mhe. Spika, masuala haya yako ya aina mbili. Kuna suala kwamba kazi hii ni ya Idara ya mazingira, wao ndio wanaostahiki kuchukua hatua ya kulishughulikia suala hili. Isipokuwa kuna utaalamu fulani hivi sasa ambao yale maji yanayotoka kwenye makaro na mvua kubwa zile, yanaingizwa kwenye mabwawa inaitwa *sewage water treatment*. Inakuwepo *pond* yanafanyiwa utaratibu, yanatiwa dawa na dawa hizo huwa hazidhuru.

Mhe. Spika, wenzetu kule Ulaya wamefika mbali kwamba maji yale wanayarejesha na kuyatumia tena, yanaingia tena kwenye mifereji na wanakuambia hasa kwamba mfereji huu maji yanayotoka unaweza kunywa. Maji yenyewe ndio hayo hayo, safari iliyotoka huko mpaka yakafikia hatua ile, unaweza kushangaa ukioneshwa mwanzo na pale yalipo, lakini bado wanakuambia ni safi kwa kunywa. Kwa sababu wanaya-*treat,* wanayatengeneza yanarudi wanayatumia.

Vile vile Mhe. Mjumbe aliendelea kusema kwamba kuna matatizo ya mambo ya viwanda. Ni kweli lakini kwa kawaida wizara inayohusiana na mazingira na wizara inayohusiana na uwekezaji, mtu yeyote anayetakiwa kuja kuwekeza kabla hajawekeza, hutakiwa kwanza uje kuchunguza mazingira kabla hujaruhusiwa kujenga kile kiwanda. Ikiwa mazingira yale na kiwanda chako kitadhuru kuweza kusababisha mazingira yachafuke, mara nyingine huwa hata kiwanda hakiruhusiwi kuanzishwa. Vyenginevyo inabidi utoe maelezo, na maelezo hayo yatosheleze kwamba uchafu ule utakaotoka kwenye kiwanda utaufanya vipi hata usidhuru.

Sasa shughuli hizi nyengine ni kweli zinahusu mazingira ya afya ya jamii, lakini yana idara zake na idara zinazohusika ni idara ya mazingira. Vile vile Mhe. Mjumbe aliendelea kuzungumzia habari ya hewa ya *oxygen* tunayovuta na tunaipatia misitu hewa ya *carbon dioxide*. Hili ni suala vile vile la idara ya mazingira, lakini kwa kweli ni suala la kitaifa.

Mhe. Spika, inasikitisha kwamba kumekuwa na utamaduni sote pengine hata na mimi, tukitaka kujenga cha kwanza pale kwenye kiwanja ni kuhakikisha kuwa hakuna mti. Sasa imekuwa ule mti unakuwa adui, kumbe ule mti ulikuwa uwe ndio rafiki wa kutusaidia kupata hiyo hewa. Hii inabidi tubadilishe tabia.

Mhe. Spika, tunatembea kwa wenzetu tunakuta majengo yamejengwa ndani ya miti na ni mti ule tu ambao ulikuwa utaathiri jengo lenyewe ndio huondolewa. Lakini miti mingine yote inabaki pale kama ni rafiki wa yale mazingira. Suala hili linahitaji viongozi wa serikali tuliwekee sera.

Mhe. Spika, zamani nakumbuka sio miaka mingi kama ukitaka kukata mti, basi ni lazima upate ruhusa kwa Sheha na viongozi wa jamii ya pale. Sasa siku hizi inaonekana kila mmoja anafanya vyake. Kwa hivyo, kuna hatari tukapata matatizo, inastahiki tuwe na sera kwamba huwezi kuruhusiwa kukata mti kama hujapanda mti, na vizuri tungekuwa na sera kwamba kila mwaka Wazanzibari wote, mkubwa au mdogo apande mti mmoja na akishapanda aoneshe kaupanda wapi, ili kuhakikisha tunalinda mazingira haya Mhe. Spika.

Kwa hivyo, maoni ya Mhe. Mjumbe yalikuwa ni mazuri na ni muhimu, lakini ni maoni ambayo yako kidogo nje ya sheria hii, kwa sababu hapa tunashughulikia wataalamu zaidi kuliko ule utendaji wenyewe ambao tuliushughulikia kwenye sheria kwa wiki moja iliyopita.

Mhe. Salma yeye alitupongeza na kutupa moyo kwamba sheria hii ni muhimu na imekuja wakati unaostahiki. Suala moja ambalo lilikuwa ni muhimu kabla sijalisahau ni la Mhe. Abdalla Juma, alisema humu tulikuwa hatukueleza kazi za maafisa wa jamii. Ni kweli humu hazikutajwa kazi za maafisa wa jamii, kwa sababu kazi zenyewe zinazotaka kufanywa zimetajwa kwenye ile sheria mama yaani *public health*. Humu tunataja sifa za afisa wa jamii na masharti ya jinsi ya kufanya kazi zake. Kazi zao wanakwenda kuzikuta huko kwenye mazingira na hawa kazi yao kusema kwamba wewe fulani kutokana na ujuzi wako, basi nenda kafanye kazi mahali fulani. Kwa hivyo, sheria hii haihitaji kazi, na sheria nyingi zinazohusu wataalamu huwa zinashughulikia taratibu na sifa za kuwa mtaalamu na masharti ya kuweza kuruhusiwa kufanya kazi ile, huwa hazihitaji kazi katika sheria hii. Kwa hivyo, sheria hii ni ya wataalamu na inataja sifa zake.

Mhe. Spika, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, alisema mambo mawili. Moja ilikuwa ni tafsiri ya lugha. Tunakubaliana naye. Pili alisema kwamba atakapokuwa mtu analipa pesa hapo kwa hapo itakuwa ni dharau na kwamba itakuwa inaweza kukejeli au inaweza kuwapa watu nguvu wakaona kwamba aah! Kumbe nitalipishwa hapo kwa hapo. Lakini hili nakumbuka tulipokuwa tunaijadili ile sheria Mhe. Mwanasheria Mkuu, alilitolea ufafanuzi kwamba huko nyuma masuala haya yaliambatana na zile shughuli za kuudhi. Tulizitaja hapa shughuli za kuudhi kwamba ilifika hatua wananchi wanafanyiwa karaha. Jirani anapiga kelele, anawaghasi kwa kupiga muziki, jamii pale inakusanyika na wanakwenda kumfikisha kunakohusika na anatiwa adabu hapo hapo, hapana kungojea urasimu kwamba sheria ichukue muda gani.

Mhe. Spika, nakumbuka juzi moja kuna mahali tulikuwa kwenye semina, Mwanasheria mmoja akasema, haya makesi yamekusanyika yanarundikana mengi. Akaambiwa hilo ni tatizo lenu kwa sababu shughuli yenyewe urasimu umekuwa mwingi. Kesi ya kuku inachukua miezi sita kutafuta ushahidi. Kwa hivyo, suala la papo kwa papo limekusudia kurahisisha kutoa adhabu kwa wale wanaoudhi kwa mambo yale yaliyokuwa yanaghasi jamii, kulikuwa hakuna nia mbaya.

Mhe. Hija Hassan Hija alikuja na mambo mawili

Mhe. Spika: Mhe. Waziri kabla hujaendelea kwa Mhe. Hija Hassan kutoa majibu. Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wote walioko nje waingie ndani, na niwaombe wanadhimu wa kila upande wasaidie kufanya kazi hiyo. Akiwa ni Mhe. Abdalla Juma Abdalla Mnadhimu wa upande wa CUF na Mhe. Salmin Awadh Salmin Mnadhimu wa upande wa CCM wawatake Wajumbe kuingia ndani. Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, nakaribia kumaliza. Mhe. Hija Hassan alishauri kuna neno zawadi pale, akasema zawadi inaweza kusababisha rushwa. Tumekubaliana na wenzangu na tutamshauri Mhe. Mwanasheria kwamba lile neno ‘zawadi’ kwenye kile kifungu tulifute kabisa, liwe halimo ili lisiharibu ile dhamira njema iliyokusudiwa na kifungu kile.

Kifungu kinasema, “fedha na rasilimali za Baraza zitatokana na michango, ruzuku na zawadi ambazo Baraza litapokea kwa mtu au taasisi”. Tumekubaliana lile neno ‘zawadi’ litoke pale, ili lisiharibu ile nia njema iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, suala la usafi ni suala ambalo linahitaji usimamizi mkubwa sana, na hivi karibuni Mhe. Spika, nilikuwa India. Moja katika nchi ambazo zinasemwa kwamba ni chafu basi ni India. Lakini kutokana na ukakamavu wa viongozi wa nchi ile, mimi nilikuwa na wenzangu wawili. Nilikuwa na Dk. Malik na Dk. Shahib, tulishangaa jinsi nchi ile ilivyobadilika sasa hivi na ikawa iko safi kinyume na maelezo yaliyokuwa yamezoeleka.

Vile vile Mhe. Spika, nilipata nafasi ya kusoma Japan. Japan walifikia hatua humu ndani kama mungekuwa na viboksi kama saba mpaka vinane ni vya kutupa taka tu humu ndani. Yaani popote unaposimama kwenye barabara ya Japan, ukizunguka nyuma utakuta kuna mahali pa kutupa taka. Mhe. Spika, kiasi cha kwamba sisi wengine tumekaa pale miezi mitatu na mpaka leo tabia ile tumekuwa nayo. Nikichana karatasi hata nikikaa kitako pale basi naitia mfukoni kwa kuogopa kwamba nikiitupa pale nafanya uchafu. Kwa hivyo, mazingira ya usafi wa jamii itategemea ni jinsi gani tumesimama kuwasimamia hawa, na tumesimama kuitekeleza ile sheria.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, maelezo mengine yalikuwa ni kusisitiza umuhimu wa kusimamia sheria na wengine walitupongeza. Kama kuna Mjumbe nitakuwa nimemsahau naomba pale itakapofika kwenye kifungu, basi niko tayari kutoa ufafanuzi ili kurahisisha maelezo haya. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama nilivyoahidi. Hebu Katibu nisaidie idadi ya Wajumbe waliopo kwa kuwahesabu. Wajumbe waliopo nje waje haraka, tunawahesabu Wajumbe waliopo ndani ili tuone kama tunatimiza wajibu wetu kumaliza kazi hii au la. Tunahesabu Wajumbe, ili tuone kama tunatimiza wajibu wetu vizuri kwa mujibu wa Katiba waingie ndani na waingie kwenye hesabu.

Katibu: Mhe. Spika, bado Wajumbe hawajatimia.

Mhe. Spika: Haya. Kama kuna Wajumbe haraka haraka waingie kabla sijatoa uamuzi wa kuakhirisha kikao hiki. Hakuna Wajumbe wengine nje.

Hebu tuhesabu tena. Ehe! Wapo wajumbe 39. Katibu soma Katiba juu ya *composition* ya Baraza hili. *Composition* ya Baraza Wajumbe gani ni Wajumbe wa Baraza kwa mujibu wa Katiba.

Katibu: Mhe. Spika, ibara ya 82(2) inaeleza kuwa :

> "Bila ya kuathiri masharti yaliomo katika kifungu cha 80 cha Katiba hii, idadi ya Wajumbe kufanya mkutano itakuwa nusu ya Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi".

Wajumbe waliopo ni 39 ni chini ya nusu Mhe. Spika.

Mhe. Spika: *Composition* ya Baraza inasemaje. Hebu tusaidieni Waheshimiwa Wajumbe. Pia tuendeni kwa mujibu wa Katiba. Tusaidiane Wajumbe wote *composition* ya Baraza kwa mujibu wa katiba, iko kwenye ibara

Katibu: Mhe. Spika, nafikiri tungeakhirisha kwa dakika tano kama inavyosema Katiba, baadae tukija tuendelee.

Mhe. Spika: Sasa tunaakhirisha kwa dakika tano, wahudumu wapige kengele ili tuone Wajumbe wamerudi na tuendelee na kazi.

Waheshimiwa Wajumbe, naakhirisha kikao hiki kwa muda wa dakika tano kama kanuni inavyosema, kengele ipigwe ili tuone Wajumbe waliopo nje wote wanaingia ndani ili tuweze kukamilisha kazi hii kwa mujibu wa taratibu za kanuni na Katiba. Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni.

(Baraza liliakhirishwa kwa muda wa dakika tano)

(*Baada ya muda Baraza lilirudia*)

Mhe. Spika: Katibu nihisabie Waheshimiwa Wajumbe waliopo

Katibu: Wajumbe 44 ni zaidi ya nusu. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, ukiangalia Katiba chini ya ibara ya 64 Wajumbe huko muko 44 na Mjumbe ambaye yupo kitini kwa mujibu wa ibara hiyo ya 64 ni wa 45, kiwango hichi kinatosha kufanya maamuzi. Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kuitikia hilo. *(Makofi)*
Lakini kabla ya kuhoji nataka niseme maneno yafuatayo. Waheshimiwa Wajumbe, nataka niwasihi sana kwamba chombo hichi ndicho kinachotoa Uongozi wa nchi, Baraza la Wawakilishi. Hichi ni chombo cha wananchi na wananchi tunawawakilisha sisi kufanya shughuli kwa ajili yao na mamlaka hasa ni yao wao.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa makubaliano ya Katiba na taratibu zetu nyengine tukasema basi hatuna nyumba ya kuwakusanya wananchi wote kufanya mambo yetu na kimsingi itakuwa ni jambo ambalo si rahisi kutekelezeka.

Kwa hivyo, busara za nchi mbali mbali pamoja na nchi yetu tukasema basi tuwe na utaratibu wa uwakilishi. Kwa maana hiyo, kuna Wajumbe wa kuchaguliwa kutoka kwenye majimbo na idadi yao ni 50, ukienda kwenye ibara ya 64 ya Katiba inatoa mchanganuo wa Wajumbe wanaofanya Baraza la Wawakilishi.

Kutokana na kifungu cha 65 cha Katiba kuna Wajumbe wa kuchaguliwa ambao idadi yao tunaijua ni 50, na ninashukuru kwa hivi sasa majimbo yote yanayo Wajumbe. Wajumbe wa kuteuliwa kutokana na kifungu cha 66 hawa ni Wajumbe wanaoteuliwa na Rais na idadi yao ni 10 na inafanya idadi ya Wajumbe 60 ukichanganya na wale 50.

Wajumbe wanawake wa Baraza la Wawakilishi kutokana na kifungu cha 67 tunaelewa kwamba tunayo idadi ya asilimia 40 ya Wajumbe wa kuchaguliwa ndio inafanywa Viti Maalum vya Wanawake vyote ni 20 na kimsingi wote hakuna upungufu ya hao, ukichanganya na wale 60 inakuja 80.

Spika, iwapo hatakuwa anachaguliwa kutoka kwa miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Spika mliyenaye yeye hakutokana na Wajumbe nyinyi, kwa hiyo na yeye atakuwa ni Mjumbe kwa mujibu wa Katiba hii. Vile vile Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar kutokana na kifungu cha 55(3) cha Katiba hii na Mwanasheria Mkuu wetu ndiye huyu hapa.

Waheshimiwa Wajumbe, nilitoa shukurani huko nyuma kwamba namshukuru sana Mhe. Rais kutimiza idadi halisi ya Wajumbe wa Baraza hili kwa mujibu wa Katiba. Wajumbe jumla 82 na nusu yake ni 41.

Kwa hivyo, nashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwamba tumeitana kwa sababu ya kuelewa umuhimu wa kufanya shughuli zetu na tumefikia wajumbe 45 ukichanganya na Spika, ambaye hakutokana miongoni mwa Wajumbe nyinyi.

Sasa serikali yetu ni ya mfumo wa umoja wa kitaifa na sisi wote tunahusika na serikali hiyo, isipokuwa tu kwa taratibu zetu inaongozwa na kile chama ambacho kilipata kura nyingi wakati wa uchaguzi, Chama cha Mapinduzi kinaongoza, lakini tunashirikiana na upande wa wenzetu.

Madhumuni makuu ilikuwa ni kuifanya nchi yetu hii iende kwa amani na utulivu na hilo ni kwa upande mmoja. Pili serikali ipate nafasi ya kufanya maendeleo ya wananchi, yakiwa pamoja na maendeleo ya jamii, kiuchumi na hata na maendeleo ya siasa zetu yaende vizuri.

Historia tunayo nyuma tena hata kabla ya kuja kwenye mfumo huu, yaani huko nyuma zaidi kabla ya mapinduzi tumekuwa na misuguano ya aina kama hii ya vyama vya siasa, na ndio iliyotufikisha mwaka 2010 kuamua baadhi yenu mtakumbuka tulikuwemo ndani ya Baraza hili na tukatengeneza utaratibu huu wa mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ili isaidie kuleta maendeleo ya wananchi.

Sisi uheshimiwa wetu tunaoitwa umetokana na wananchi kwa kukubali Katiba hii ndio tukaitwa Waheshimiwa Wajumbe, tumeitwa Waheshimiwa Wajumbe kwa ajili hiyo. Wananchi wameamua kutuchagua nendeni huko mkatuzungumzie masuala yetu. Kwa hivyo, itakapofika pahala kama hatutimizi wajibu wetu narudia yale maneno ambayo tunasema humu Barazani kwamba tutakwenda kuulizwa.

Waheshimiwa Wajumbe, maneno yale kila mtu ajiusie mwenyewe kwamba iko siku tutakwenda kuulizwa namna gani tumetimiza wajibu wetu katika kuendeleza maisha ya wananchi. Hatukufanya hivyo, basi tukubali kwamba tutakwenda kujibu mbele ya Mwenyezi Mungu na sote tuna imani juu ya masuala haya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nakuombeni kuwa tutimize wajibu wetu kama wananchi walivyotutaka kwa mujibu wa Katiba hii tuwatekelezee mambo yao, vyenginevyo itakuwa hatutimizi wajibu wetu, ambayo hiyo itakuwa ni kinyume na Katiba. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana kwa kunisikiliza maneno haya ambayo ni muhimu, ili tuone nchi yetu inakwenda. Vile vile nitumie nafasi hii kuwaomba wananchi wajenge utamaduni wetu wa kawaida wa kuelewana na watu wa nchi hii wote ni wamoja, tutunze amani na usalama ndani ya nchi. Viongozi mbali mbali wa kidini pamoja na wengine sote tutakwenda kuulizwa suala hilo hilo. Kwa kweli maneno haya nayasema kutoka ndani ya moyo wangu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nakuusieni nyinyi Waheshimiwa viongozi pamoja na viongozi mbali mbali wa kidini, kwamba tujiusie wenyewe kuwa tutakwenda kuulizwa siku moja mbele ya Mwenyezi Mungu juu ya suala hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana.

Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na Mhe. Waziri, naomba sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria, ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira ya 2012

Sehemu ya Kwanza
Utangulizi

Kifungu 1 – Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2 – Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Pili
Kuanzishwa kwa Baraza

Kifungu 3 – Kuanzishwa kwa Baraza
Kifungu 4 – Muundo wa Baraza pamoja na marekebisho yake
Kifungu 5 – Kazi za Baraza
Kifungu 6 – Uwezo wa Baraza pamoja na marekebisho yake
Kifungu 7 – Mafunzo ya Afya ya Jamii pamoja na marekebisho yake
Kifungu 8 – Vikao vya Baraza
Kifungu 9 – Akidi ya Mkutano
Kifungu 10 – Uwakilishi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 11 – Maoni ya Baraza pamoja na marekebisho yake
Kifungu 12 – Amri na maelekezo mengine ya Baraza
Kifungu 13 – Malipo kwa Wajumbe
Kifungu 14 – Kumbukumbu za kikao

Sehemu ya Tatu
Usajili na Utoaji Leseni

Kifungu 15 – Mrajis wa Baraza pamoja na marekebisho yake
Kifungu 16 – Kazi za Mrajis pamoja na marekebisho yake
Kifungu 17 – Usajili na utoaji leseni pamoja na marekebisho yake
Kifungu 18 – Malipo ya usajili na leseni
Kifungu 19 – Kuomba tena leseni pamoja na marekebisho yake
Kifungu 20 – Usajili wa wageni pamoja na marekebisho yake
Kifungu 21 – Usajili wa muda pamoja na marekebisho yake
Kifungu 22 _ Uwezo wa kusitisha, kufuta na kuondoa usajili pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Nne
Masharti ya Adhabu

Kifungu 23	–	Mrajis kupokea malalamiko pamoja na marekebisho yake
Kifungu 24	–	Uchunguzi wa Baraza
Kifungu 25	–	Taratibu za uchunguzi
Kifungu 26	–	Uwezo wa Baraza wa kutoa adhabu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 27	–	Uwezo wa kuita shahidi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 28	–	Kinga kwa shahidi
Kifungu 29	–	Rufaa dhidi ya uamuzi wa Baraza pamoja na marekebisho yake
Kifungu 30	–	Kuwasilisha shauri Mahakamani pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tano
Makosa na Adhabu

Kifungu 31	–	Adhabu kwa kufanya kazi bila ya ruhusa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 32	–	Makosa kwa kujipatia usajili na leseni kinyume na utaratibu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 33	–	Adhabu kwa wasioheshimu maagizo ya Baraza
Kifungu 34	–	Adhabu ya ujumla
Kifungu 35	–	Adhabu bila ya mashtaka pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Sita
Masharti ya Fedha

Kifungu 36	–	Chanzo cha fedha pamoja na marekebisho yake
Kifungu 38	–	Ukaguzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 39	–	Uwezo wa Waziri kutunga Kanuni

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla Baraza kurudia Mhe. Mwanasheria Mkuu aliniarifu kwamba atakuwa na maelezo ya jumla kuhusu mpangilio wa vifungu. Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Kwa ufupi ni kwamba kwa kawaida tunapoandaa sheria pia kuna mtiririko wake ambao tumejizowesha katika kutunga au kuandaa sheria, ambao kwa bahati mbaya katika maandalizi tulipitikiwa.

Kwa mfano, mtakuta kwamba masharti ya fedha yamekuja mwishoni mwa sheria hii, yaani imekuwa hivi sasa ni sehemu ya sita ya sheria, wakati kawaida vifungu vilivyopo katika sehemu ya tano kuhusiana na makosa na adhabu ndio vilitakiwa vije mwisho wa hii sheria.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti ningependekeza kwamba tufanye marekebisho ya mtiririko wa vifungu, ili tutakapoipeleka kwa Mhe. Rais kwa ajili ya kupata idhini tuwe tumempelekea kitu ambacho ni kizuri, kwa sababu kwa kawaida tungeweza au Mwanasheria Mkuu chini ya Sheria Nam. 16 mwaka 1961 anao uwezo wa kuvipanga tena vifungu katika sheria, lakini ni baada ya Mhe. Rais kuweka saini. *(Makofi)*

Sasa mimi nadhani kwa sababu hii ni sheria yetu baada ya kuipitisha hapa tumpelekee kitu ambacho tumekipanga kwa uratatibu ule ambao tumejiwekea. Kwa maana hiyo, napendekeza kwamba vifungu vyote vya sehemu ya sita isipokuwa kifungu cha 39 viwe ni sehemu ya tano ya mswada huu au sheria hii tutakapoipitisha, na vifungu vyote vya sehemu ya tano ndio viwe vifungu vya sehemu ya sita ukichanganya na kile kifungu cha 39.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya marekebisho hayo tutakuta mtiririko wa vifungu utakuwa kama ufuatavyo:-

Kifungu cha 36 kitakuwa cha 31,

Kifungu cha 37 kitakuwa cha 32,
Kifungu cha 38 kitakuwa cha 33,
Kifungu cha 31 kitakuwa cha 34,
Kifungu cha 32 kitakuwa cha 35,
Kifungu cha 33 kitakuwa cha 36,
Kifungu cha 34 kitakuwa cha 37,
Kifungu cha 35 kitakuwa cha 38 na
Kifungu cha 39 kitabaki kuwa cha 39.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wakubali marekebisho haya ya mpangilio wa vifungu, ili tutengeneze sheria nzuri.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, tuliwasiliana, kujadiliana na tukakubaliana. Kwa hivyo, nakubali ushauri wa Mhe. Mwanasheria Mkuu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunakubaliana na marekebisho hayo madogo ya mtiririko wa vifungu. Tunashukuru.

Baraza lilirudia

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira ya 2012

(Kusomwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira ya 2012 usomwe mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake kusomwa kwa mara ya tatu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikal ulisomwa mara ya tatu nai umepitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nikushukuruni kwa mashirikiano makubwa ya kutekeleza shughuli zetu.

Vile vile tunakumbuka kwamba kwanza leo ni siku ya Ijumaa, lakini tulijipangia kuwa mnamo saa 8 za mchana, nadhani kuna wale wataalamu kutoka Chuo Kikuu kuhusiana na ombi letu Tanzania kuongezea eneo la upeo wa Bahari Kuu. *(Makofi)*

Kwa kweli tulisema kwamba jambo hili Wajumbe tulitaka tulijadili, lakini ni jambo kubwa tena ni pana na linahusu utaalamu. Kwa hivyo, tuliwasiliana na Mhe. Waziri na alisema tumtafutie nafasi, ili tuje tupeane maarifa juu ya jambo hili. Kwa maana hiyo, Mhe. Waziri yupo tayari na leo ni siku ya Ijumaa na hivi sasa ni saa 5, basi nadhani tukubaliane kwamba tuifanye kazi hiyo mnamo saa 8 za mchana baada ya kutoka kusali sala ya Ijumaa. *(Makofi)*

Sasa kama hivyo ndivyo, basi nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote kwa umuhimu wa jambo lenyewe tukutane pale ukumbi wa juu saa 8 za mchana. Lakini kwa mnasaba wa shughuli za Baraza naakhirisha kikao hichi na tusitishe shughuli zetu, na kwamba jioni ya leo tusije kwa shughuli za Baraza, lakini tuje kwa shughuli za semina. Kwa maana hiyo, basi niakhirishe kikao hichi hadi siku ya Jumatatu tarehe 22/10/2012, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 5:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 22/10/2012 saa 3:00 za asubuhi)